

Penina Muhando
1974
HESHIMA YANGU
East African Publishing House,
Lusaka Close, SLP 30571, Nairobi

Nacherzählt von
Lourenco Noronha
Lektor (1974-2009) für Swahili-Literatur
am
Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien
Taasisi ya Taaluma ya Bara la Afrika
Chuo Kikuu cha Vienna

Stand: Mai 2009

Widmung
Kutabaruku

al-hamdu li-llahi
subhanahu wa-ta'ala

Dibaji
Vorwort

Angeregt wurden diese didaktischen Unterlagen von Studierenden am Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien.

Die deutschsprachigen Teile wurden von Dr. Franz Rader korrigiert; dieser hat während seiner Tätigkeit an der Österreichischen Botschaft in Nairobi meine Berufung nach Wien gefördert. Für beides bin ich ihm dankbar.

Lourenco Noronha
E-mail: noronha@gmx.at

1. Einleitung
Utangulizi

1.1. Autorin: Biographische Notizen
Wasifu ya mtunzi

Penina Muhando, verheiratete Mlama, wurde am 3. März 1948 in Kilosa, Tanganyika (seit 1964 Tansania) geboren. Sie studierte Theaterwissenschaft an der Universität Dar-es-Salaam und lehrte nach Abschluß ihres Studiums dort (*Idara ya Sanaa za Maonyesho*). Sie gehört zur ersten Generation der Autoren nach der Unabhängigkeit (1961) und war maßgeblich daran beteiligt, Swahili-Theater afrikanisch und entwicklungspolitisch zu gestalten. In der Einführung zu ihrem Buch Culture and Development. The popular Theatre Approach in Africa schreibt sie: "The reflections in this book are a result of a decade's theoretical and practical preoccupation with popular theatre in relation to development." (S. 5). Ihre Theatertexte werden in Schulen und an Volksbühnen aufgeführt. Sie kommen gut an, weil sie volks- und lebensnah sind.

1.2. Thematische Einführung
Kiini (dhamira, dhana, mada, wanda/ma-) maalum

„*Kiini chake ni mapenzi baina ya mvulana na msichana (...). Mzee Isa, baba wa msichana (...) anapinga uchumba huo (...).*“¹

Heshima Yangu wurde vor dem Theatertext Hatia verfaßt, aber nach diesem veröffentlicht. Die Handlung dieses ihres ersten Theaterstückes ist gradlinig und übersichtlich. Die Zufälligkeiten sind zwar zielführend, aber unglaubwürdig. Schon in diesem Text zeigt Muhando ihre Tendenz zu einer personen- und milieuspezifischen Sprache mit Einfühlungsvermögen für psychologische Aspekte der Frauensprache, was besonders im Gespräch zwischen Rukia und ihrem Bruder Hamza (S. 8-9) sowie in der Schlußrede Mama Salums (S. 19) zum Ausdruck kommt. Auch schon in diesem ersten Stück kommt Muhandos Humor² zum Vorschein, der so wie bei Edwin Semzaba³ und bei Ngalimecha Ngahyoma⁴ einen einzigen Nachteil hat: Er regt nicht zum Lachen an.

Mzee Isa gehört zum Rat der Ältesten seines Dorfes. Seines Alters und seines Amtes wegen genießt er den Respekt der Dorfbewohner. Sein persönliches Leben wird aber von der Autorin in Frage gestellt.

Das Grundthema dieses Textes ist meines Erachtens die Rechte und Würde der Frauen. Daß eine Frau ihre Rechte einfordert, kommt in der Swahili-Literatur selten vor.

1.3. Literaturhinweise
Marejeo

Die Zahlen in Klammern beziehen sich auf die jeweilige Signatur der Fachbibliothek für Afrikawissenschaften und Orientalistik der Universität Wien.

¹ Rückseite des Umschlags

² Siehe z.B. die Parodie über den *Mganga* in Hatia (S. 24-29) und den Zank zwischen den Frauen in Nguzo Mama.

³ Tausi wa Alfajiri, S. 55-60

⁴ Kijiji Chetu, S. 29-31

1.3.1. Primärliteratur

- Muhando, Penina. 1976 (1972). Hatia. Nairobi: EAPH. 41pp. (B.8.9.1.).
- Muhando, Penina. 1980 (1973). Tambueni Haki Zetu. Dar es Salaam: TPH 34pp. (B.8.9.15.).
- Muhando, Penina. 1974. Heshima Yangu. Nairobi: EAPH. 19 pp. (B.8.9.8.).
- Muhando, Penina. 1987 (1975). Pambo. Nairobi: Foundation Books/ Dar es Salaam: Swala Publications. 56pp. (B.8.9.20.).
- Muhando, Penina. 1976. "Talaka si Mke Wangu", in: (ed.) Mbonde, J.M. Uandishi wa Tanzania. Michezo ya Kuigiza. Nairobi: EALB. S. 96-121. (B.8.9.38.).
- Muhando, Penina. 1982. Nguzo Mama. Nairobi: OUP. 59pp. (B.8.9.34.).
- Muhando, Penina. 1984. Lina Ubani. Dar es Salaam: DUP. 59pp. (B.8.9.78.).

1.3.2. Sekundärliteratur

- Balisidya, May. 1987. "The construction of Sex and Gender Roles in Penina Muhando's Plays", in: Kiswahili. Dar es Salaam: IKR. 54/1+2, S. 34-38. (Z.1.10.54/1+2.).
- Mbise, Ismael R. Date. "Hatia. Mapitio ya Mchezo wa Kuigiza⁵", in: Kiswahili. Dar es Salaam: IKR. 41/1, S. 165-167. (Z.1.10.41/1.).
- Mbunda, Msokile. 1991. Uchambuzi na Uhakiki "Lina Ubani". Dar es Salaam: DUP. (B.8.20.61/4.).
- Mponda, M.S. 1977. (Review) "Tambueni Haki Zetu", in: Mulika. Dar es Salaam: IKR. 10, 20-26. (Z.1.11.10.).
- Mugo, Micere Githae. 1976. "Gerishon Ngugi, Penina Muhando and Ebrahim Hussein. Plays in Swahili", in: African Literature Today. London: Heinemann. 8, S. 137-141. (Z.3.1.8.).
- Muhando (Mlama), Penina 1973. Music in Tanzanian traditional Theatre. Dar es Salaam: University. M.A. Thesis.
- Muhando, Penina. 1975. "Modern African Theatre with special Emphasis on East Africa", in: Umma. University of Dar es Salaam. V,1, S. 1-11.
- Muhando, Penina. 1979. The Role of Women in Culture Reproduction: The Case of Tanzanian Art and Literature. Paper Nr. 17. BRALUP Workshop on Women's Studies and Development. University of Dar es Salaam. Sept. 24-29, 1979.
- Muhando, Penina. 1983. Tanzanian traditional Theatre. Dar es Salaam: University. Dissertation.
- Muhando, Penina. 1986. The major Trends in Tanzanian Theatre Practice. Paper presented at the Jahnheinz Jahn Symposium, Mainz.
- Muhando, Penina. 1990. "Creating in the Mother-tongue: The Challenges to the African Writer today", in: RAL. Bloomington: IUP. 21-4, S. 5-14. (Z.3.4.21-4.).
- Muhando, Penina. 1991. Culture and Development. The popular Theatre Approach in Africa. Uppsala: The Scandinavian Institute of African Studies. 219pp. (S.7.0.46.).
- Muhando, Penina. 1991. "Women's Participation in 'Communication and Development': The popular Theatre Alternative in Africa", in: RAL. Bloomington: IUP. 22/3, S. 4.
- Sengo, Tigiti. 1977. (Review) "Pambo" in: Mulika. Dar es Salaam: IKR. 11, S. 46-59. (Z.1.11.11.).

⁵ Der Begriff *Mchezo wa Kuigiza* ist durch *Tamthilia* ersetzt.

2. Texte
Matini

2.1. Personen
Wahusika

Hadija⁶: Rukias Freundin
Hamza⁷: Rukias Bruder, 20 Jahre alt
Mama Salum: Salums Mutter, 43 Jahre alt
Mzee Isa⁸: Rukias Vater, etwa 49 Jahre alt
Rukia⁹: Ein 18jähriges Mädchen
Salum: Rukias Freund, 25 Jahre jung
Tatu
und Asha: Freundinnen Hadijas

2.2. Theatertext
Tamthilia

2.2.1. Onyesho la kwanza.

Hadija und Rukia befinden sich vor Mzee Isas Haus. Rukia worfelt Mais. Hadija kommt mit einem Wassereimer an der Hand. Sie plaudern über ihre Arbeit und über Rukias Freund Salum.

Hadija: Rukia! Hivyo mahindi yote yale uliyotwanga (uliyoyatwanga) jana hayakutosha, bado unaongeza mengine?

Rukia: La! Hadija wangu. Namaliza kupepeta haya ambayo niliachilia jana. Niliyotwanga (niliyoyatwanga) yalikuwa mengi mno wala sidhani kama nitalazimika kutwanga tena kwa muda hata wa mwezi mzima. Habari gani za huko kwenu?

Hadija: Hakuna baya. Je, vipi? Utakwenda kumwona Salum leo pia? Naliwaona (ninyi) jana mkitokea sehemu za kisimani. Ama mambo yameiva siku hizi, ee?

Rukia: Shhh! Acha kusema kwa nguvu hivyo, ndugu yangu. Unaelewa mzee akiyasikia yatakuwa makubwa hayo.

Hadija: Ala! Yatakuwaje makubwa? Hakika sioni sababu itakayomfanya Mzee Isa akasirike kusikia kuwa binti yake anapendwa na kijana mzuri Salum. Walahi mimi nisingelifanya jambo kama hilo kuwa siri.

Rukia: Tusijifanye vipofu na kutokuona ukweli wa mambo. Unasahau kuwa sisi ni wa-Bantu. Hata kama mambo kama hayo yametengemaa kati ya wawili wanaohusika, wazazi wana sheria zao za kupashwa habari, siyo kuyasikia nje nje tu. Ni jambo gani lililo geni kwako litakalonipasa nikueleze, ndugu yangu? (*Uk.7*).

⁶ Der Prophet Mohammed heiratet vier Frauen: Aisha (*prosperous*), Hadija, Maymuna (*blessed*) und Umm Habiba (*beloved*). Hadija gebahr Fatma, die den Khalifen und Nachfolger des Propheten Ali heiratete.

⁷ Hamza, genannt „Der Löwe“, war der Onkel des Propheten. Er starb A.D. 625.

⁸ Isa ist die arabischen Version des jüdischen Namens Jesus.

⁹ *Ruqa* bedeutet „pretty, beautiful“ und *Ruqya* bedeutet „charm“.

Hamza kommt aus dem Haus und steht vor der Eingangstüre. Er führt ein kurzes Gespräch mit Hadija, die es eilig zu haben scheint. Sie ist nämlich zum Fluß unterwegs, von wo sie Wasser holen möchte, um die Wäsche zu waschen. Sie verabschiedet sich mit kurzen Worten von Hamza und Rukia, entfernt sich einige Schritte von ihnen und bricht in lautes Gelächter aus. Das kommt Hamza sonderbar vor.

Hamza: Ala! Jambo gani la kuchekesha limesemwa hapa?

Rukia: (akiwa bado anashangaa) Unaniuliza nini? Na tutumaini kuwa siyo ishara za wenda wazimu. Mambo huwa yanaanza kidogo kidogo hivi hivi. Hamza, baba yuko ndani?

Hamza: Hapana, hayuko. Alitoka kitambo kidogo kwenda kukagua shamba lake lililo karibu na mikoroshoni kupitia kisimani. Vipi, unaogopa isije ikawa ameyasikia mliyokuwa mnayazungumzia? Hebu nieleze vizuri mie basi, kwa maana nimeyasikia juu juu tu. Eti Salum ndiye shemeji yangu, ee?

Rukia: (Anacheka kwa aibu huku anainama kuchukua mahindi mengine kwenye kikapu.) Acha kunitania, Salum. Dada yako mimi au huna habari?

Hamza: Kwa kweli sina madhumuni ya kukutania, dada yangu. Nitakalo ni kupashwa habari za kufurahisha, maana kupata shemeji usichukulie kama ni jambo dogo. Basi inatubidi tunaohusika kutafuta ukweli ili tuweze kujitahadhari na kupalilia unga.

Rukia: Usizidi kunitania, Hamza. Msifike mbali, wewe wala Hadija. Urafiki usichukuliwe kama ni uchumba na kama una haja sana ya shemeji kwa nini usiwe mvumilivu mpaka wakati utakapowadia. Mwenye dada hakosi shemeji, kwa hivyo wewe ngoja tu. (Uk.8).

Rukia und ihr Bruder kommen auf das Thema Brautgeld (mahari) zu sprechen, denn Rukias Heirat würde Brautgeld ins Haus bringen, welches ihm helfen würde zu heiraten. Salum seinerseits kennt seinen Vater nicht. Er müßte das Brautgeld selber verdienen. Rukia erklärt ihrem Bruder, daß zwar Mädchen heutzutage nach Geld trachten, aber zu denen gehöre sie nicht.

Hamza: Sasa kumbe wewe unanitania mimi. Afadhali ungeniambia kuwa wewe na Salum hamtegemei kuoana hivi karibuni, maana kusema kweli, Salum bila shaka anahitaji kukusanya mahari akiwa mtu mwenyewe hana baba, na kazi yenyewe ameanza hivi karibuni. Ngoja ajistawishe kwanza.

Rukia: Pesa haziwezi kumhangaisha mtu kama mimi – unajua Hamza, ingawaje watu wengi siku hizi wanasisitiza kuwa wasichana wote tunapenda pesa. Hakika si wote walio hivyo. (Uk. 9).

Mzee Isa ist in der Nähe, aber Rukia und Hamza haben ihn noch nicht gesehen. Sie führen inzwischen das Gespräch weiter, worin Hamza seine Befürchtungen zum Ausdruck bringt, daß sein Vater viel Geld von Salum verlangen werde. Plötzlich steht Mzee Isa vor ihnen. Er hat alles gehört. Rukia ist sehr verlegen und weiß nicht, was sie tun soll. Sie versucht ins Haus hinein zu flüchten.

Mzee Isa: (Anamkaribia Rukia.) Simama wewe kule. Habari gani hizi juu ya harusi za kina Salum?

Hamza: Tunaongea tu, mzee.

Mzee Isa: Acha kunidanganya sikuzaliwa jana wala leo. (Anamtazama Hamza kwa hasira, halafu anamtazama Rukia.) Jinsi anavyokuwa (anavyokua?) mtoto na

adabu zake zinapungua vile vile. Unavuka mpaka sasa. Walahi, Rukia mwanangu, unavuka mpaka kabisa. Yaani natarajia kuwa siku moja nitakuja kuarifiwa kuwa unataka kuolewa na Salum! Salum! Salum, mwana haramu¹⁰ yule! Huku ni kutaka kunivunja heshima yangu. Niambie, wee mtoto, umeshawahi kukutana na baba-mjomba, angalau baba-shangazi wa Salum. Hana. Haikutosha ile baa ya kutokuwa na baba, akakosa hata ndugu wa kiume. Na wewe ndiye unachagua kuolewa naye? Loo! Nani anayetaka harusi yenye sherehe nusu-nusu? Nani atasimamia sherehe upande wa baba wa Salum? Hata kidogo siwezi kumwoza binti yangu kijana namna hii.

Hamza: Lakini mzee, nafsi ya Salum ina kosa gani kwa kule kutokujua baba yake au kukosa ...

Mzee Isa: (Amkatisha kwa kumkemea.) Sitaki upuuzi huo. Naona genge lenu moja na dada yako. Acheni kunivunja heshima yangu, watoto. Nilipita kisimani nikiwasikia wale wasichana rafiki zako wakicheka juu ya jambo hili. Siwezi kukubali kudharauliwa hata na visichana vidogo (*Anamnyooshea kidole Rukia.*) Nisikusikie ukiendeleza mambo haya. Na yaishie hapo yalipofika. (*Aelekea ndani.*) Hamza, nitafutie panga langu nikakate miti. (*Anaendelea.*) Heshima yangu watoto. (*Uk. 9-10*).

Rukia überlegt.

Rukia: (Anasogea mbali na nyumba anawaza kwa huzuni) „Heshima yangu, heshima yangu“. (*Kimya kwa muda*) Ni heshima gani ipatikanayo katika kumkatalia furaha kijana mzuri, mwenye tabia nzuri na moyo wa imani, eti kwa sababu ni mwana haramu. Ni kosa la nani Salum kutokujua baba yake? Ni kosa la nani mama yake Salum kuzaliwa peke yake, hivyo kumnyima mwanawe mjomba? (*Asema pole pole.*) Hana baba, hana mjomba, hana baba-shangazi, kwa hivyo sherehe za harusi si kamili. Sherehe za harusi ni heshima kuliko furaha ya maisha ya binadamu asiye na kosa. (*Uk. 10*).

Rukia schweigt und senkt den Kopf. Sie denkt weiter nach.

Rukia: Lakini kwa sababu gani akina Hadija wacheke juu ya urafiki wetu na Salum. Leo hii tu Hadija alielekea kama anayenitakia mema. Ni kweli wengi wanamlilia Salum lakini huku kucheka sielewi kunakuja namna gani. (*Anaelekea kwenye kikapu.*) Maskini Salum, nitawezaje kumweleza sababu anazozitoa mzee kuvunja urafiki wetu. (*Uk. 10*).

Mzee Isa, der sich heimlich heranmacht, unterbricht ihre Überlegungen.

Mzee Isa: Una wazimu mtoto wewe. Unabwata nini peke yako? (*Anamtishia panga.*) Acha masihara Rukia na kuondoa upuuzi wa mwana haramu wako. Unanielewa mimi nilivyo, ama siyo? Usidhanie kwa vile mama yako hayupo basi unaweza kufanya unalopenda (unalolipenda) bila kuzuiwa. Ndivyo maana siku hizi kazi kaziendi vizuri hapa nyumbani. (*Uk. 10*).

¹⁰ Ein Kind, das außerhalb einer rechtmäßigen Ehe geboren wird, wird in Kiswahili *mwana haramu* genannt. *Haramu* steht im Gegensatz zu *halali*, was „erlaubt“ and „rechtmäßig“ bedeutet. Da *haramu* im islamischen Kontext auch für Schweinefleisch verwendet wird, empfehle ich den Begriff *mwana haramu* nie zu verwenden.

Er befiehlt ihr sich mit dem Haushalt zu beschäftigen, Wasser zu holen und den Mais zu stampfen. Rukia geht ins Haus hinein und Mzee Isa geht aufs Feld.

2.2.2. Onyesho la pili.

Rukia kommt mit einem Kübel voll Wasser vom Dorfbrunnen zurück. Sie geht langsam und ist in Gedanken versunken. Salum kommt ihr entgegen, aber es braucht ein wenig Zeit, bis sie ihn wahrnimmt. Er möchte aber mit ihr über das, was ihm am Herzen liegt, sprechen. Er versteht auch nicht, warum sie plötzlich so zurückhaltend geworden ist.

Salum: He! Makubwa haya! Una nini, Rukia? Ikiwa unaona ndoo inakuelemea kwa nini usiitue au hata mimi naweza kukubebea mradi uniruhusu niseme nawe. Niko tayari kukujulisha hali yangu lakini mwishoni kabisa nikishaeleza yaliyo moyoni.

Rukia: Uzito wa ndoo ni jambo nililozoea, kwa hivi huna lazima yo yote kunisaidia, na iwapo hutaki kunijulisha hali yako nadhani nikuonavyo u mzima kwa hiyo nakwenda. (*Aanza kwenda.*)

Salum: (*Amshika asiende.*) Rukia mpenzi, mbona hivi? Lo! Umeshabadili nia? Kwa sababu gani basi usichague njia ingine (njia nyingine/zingine) ya kunifahamisha mabadiliko ya mawazo kuliko kunifanya mimi kama mjinga hapa njiani. Unajua ni mambo mangapi ya maana nimeacha kufanya kwa kusudi la kukuona wewe? Kumbe loo!

Rukia: Hayo ni mawazo yako mwenyewe. Laiti kama ungeyafikiria unayosema (unayoyasema) kabla ya kutamka. Usiropoke, Salum, usije ukajutia nafsi yako. Kwa nini kunifanya mimi kama msichana asiye na uwezo wa kutumia akili na kuniwazia kuwa naweza kufanya mambo hivyo? Inaonekana unaniongeza uchungu nilio nao badala ya kunisaidia.

Salum: Hujaniambia, Rukia, nitajuaje kama kuna jambo linasumbua (linaloisumbua) roho yako?

Rukia: Hujaniuliza.

Salum: Nisamehe sana, lakini basi nieleze jambo lenyewe. (*Uk.11-12*).

Rukia möchte einfach nicht weiter mit Salum sprechen. Sie dreht ihm den Rücken zu. Salum gibt aber nicht nach und folgt ihr. Rukia ist so aufgeregt, daß sie den Wasserkübel auf ihrem Kopf fast verschüttet, aber Salum hilft ihr, ihn auf den Boden zu stellen.

Rukia: Nimekwambia usiropoke, Salum. (*Ageuka na kumpa mgongo.*) Nisikize, Salum. Baba yangu amesikia kwa bahati mbaya juu ya urafiki wetu. Lakini amenikasirikia sana na kuniambia maneno ya kuumiza moyo wangu.

Salum: Maneno gani, Rukia? (*Anamsogelea karibu.*)

Rukia: (*Anataka kuondoka lakini anaonekana mwenye kuishiwa na nguvu. Yuko karibu kuangusha ndoo lakini Salum aharakisha na kuitua chini.*) Sahau mapenzi yetu, Salum.

Salum : (*Akodoa macho kwa mshangao.*) Sema tena, Rukia.

Rukia: Usinifanye mimi kama mwaaji. Maneno niliyosema (niliyoyasema) na ambayo sitaki kuyarudia si amri yangu ila ya baba yangu. Amenitishia vikali kama sitaukomesha urafiki huu hapa ulipofika.

Salum: (Anauma kidole na kumpa Rukia mgongo.) Mama yangu wee! Hivyo naota au ni kweli? Sema tena, Rukia, sema tena, Rukia, labda sikusikia vizuri. Sema, sema!

Rukia: Eti niseme tena. Nitapata faida gani kurudia maneno yavunjayo moyo wako na wangu pia? Lakini wangu ulishavunjika kitambo. *(Anakaa chini.)*

Salum: (Amwendea Rukia.) Sielewi, Rukia. Ni sababu gani aliyoitoa mzee?

Rukia: (Anataka kuinuka.) Niache niende, Salum, siwezi kukaa hapa zaidi. Nisamehe. Wewe unajua kuwa nilikupenda kwa moyo wangu wote lakini kumbe wazazi waweza kuwa kipingamizi kikubwa cha furaha ya maisha ya mtu. Nitakwenda nyumbani sasa. *(Anajaribu kuinuka lakini Salum anamzuia.)*

Salum: Utanieleza kwanza kabla sijakuacha uondoke hapa. *(Anamshika mkono.)* Nieleze yote tafadhali, labda naweza kutafuta njia ya kumshawishi mzee kubadili nia yake. (...) *(Uk. 12-13).*

Ganz unerwartet kommt Mzee Isa vorbei. Er trägt Brennholz und hat ein Buschmesser bei sich. Als Salum Rukia „Rukia mpenzi“ (uk. 13) nennt, steht Mzee Isa vor ihm. Er rügt Rukia. Salum nimmt sie in Schutz.

Salum: (kwa woga) Mzee, hayo ni makosa yangu; ni mimi niliyem... .

Mzee Isa: (kwa ukali) Kelele, mwanaharamu wee! Kwanza huna hata haya kunisemesha baada ya kufanya haya. Ingekuwa kichwani zimo ungeona afadhali kukimbia kuliko kubaki kungoja ghadhabu yangu. Toto lisilo na baba! Unathubutuje kumsogelea mtoto wangu mimi?

Rukia: (Anabeba ndoo na kukimbia nayo.) Sitaki kuyasikia maneno hayo tena, baba. *(Anapotea.) (Uk. 13).*

2.2.3. Onyesho la tatu.

Mama Salum sitzt in ihrem Wohnzimmer, flechtet eine neue Matte und singt dabei. Im Wohnzimmer stehen ein kleiner Tisch und drei Sessel. Sie hat für ihren Sohn seine Lieblingsspeise zubereitet, nämlich ugali und kisamvu. Doch als Salum hereinkommt, merkt die Mutter, daß etwas nicht stimmt.

Mama Salum: Vipipi, Salum mwanangu, mbona unaonekana mwenye huzuni sana? Jambo gani limekutokea?

Salum: Shikamoo, Mama.

Mama Salum: Marahaba. Lakini hujajibu swali langu.

Salum: Habari za kutwa.

Mama Salum: Nzuri, lakini kwanza nieleze shida yako, ama sivyo sitajibu swali lako lingine.

Salum: Akili zangu kazifanyi kazi sawa sawa, Mama. Niache nipumzike kidogo.

Mama Salum: Jamani, mambo gani haya. Basi kula chakula labda utajisikia afadhali. *(Ainuka kwenda kumtolea chakula kabatini.)*

Salum: Sihisi njaa, Mama, lakini ni chakula gani umetayarisha?

Mama Salum: Ugali na kisamvu, mboga yako unayoipenda. Tena leo kisamvu kimekolea nazi vizuri ajabu.

Salum: Kama ni kisamvu nitakula. *(Anakaa kwenye kiti.)* Loo salaaale! Walahi kumbe kuna wakati mtu anaweza kujiona yu mzee kabisa kwa sababu ya mikasa. Ujana wangu umenitoka leo. *(Anakula.)*

Mama Salum: Nieleze upesi, Salum, roho yangu hainitumi kubaki bila kuelewa kinachokusumbua. Tafadhali nieleze. Kama ni jambo baya la kunidharau

usiogope kusema kwa vile nimepatikana na mabaya mengi katika siku za maisha yangu. Uzee nilio nao kwa hakika siyo wa umri bali wa mikasa. (*Anamsogelea.*) Lakini tusikalie kueleza mikasa iliyokwisha pita (kupita). Hebu na tusikie hii ya leo. Sema basi.

Salum: Usiingiwe na wasi wasi, Mama. Hizi ni shida zangu mimi mwenyewe. Ngojea nimalize kula nitakueleza sasa hivi. (*Mama Salum anakaa kwenye kiti. Salum anamaliza kula na kunywa maji.*) Kwa muda wa siku nyingi kidogo nimefanya mapenzi na Rukia. (*Uk. 15-16.*)

Mama Salum ist erschrocken. In diesem Augenblick klopft Mzee Isa an die Tür.

Mama Salum: Karibu, Mzee Isa. Karibu kiti. Karibu. (*Anakaa kwenye kiti.*)

Salum: Natoka, Mama. (*Anaondoka.*)

Mama Salum: Ala! Salum mwanangu, mbona unakimbia wageni. Mbona hatujamaliza kuongea.

Salum: Nitarudi baadaye. (*Anatoka nje.*)

Mzee Isa: (*Anamtazama Salum akitoka, halafu anamtazama Mama Salum kwa muda.*) Habari za masiku?

Mama Salum: Salama. Ajabu kubwa hii. Jambo gani limekuleta hapa leo? Hujafika hapa.

Mzee Isa: Wala sikutegemea kufika hapa kwa kweli. Kwa kawaida huwa sivunji ahadi. Ni jambo la huzuni kuwa ni mimi katikati yetu ninayevunja ahadi yetu ya siku ile. Lakini mambo hutokea yasivyotegemewa, kwa hivyo uelewe kuwa si jambo la utani lililonileta hapa. Sikuwa na njia ingine (nyingine/zingine?) ila kufika.

Mama Salum: Usizungushe maneno na kuniweka katika wasi wasi. Ama kweli siku ya leo itanitia wazimu. Wasi wasi moja kwa moja. Kumetokea nini huko jamani?

Mzee Isa: Wapi?

Mama Salum: Ala!

Mzee Isa: Tulia, tulia, mimi nitasema tu, wala usidhanie nina haja ya kukaa hapa muda mrefu mrefu. Ni kinyume cha dhamira yangu kabisa. Lakini ... (*Ananyamaza na kufikiri.*) ni juu ya hawa watoto. (*kimya*). (*Uk. 16-17.*)

Mama Salum wird stutzig. Sie fordert Mzee Isa auf, offen zu sprechen.

Mama Salum: Watoto gani?

Mzee Isa: Hawa watoto wetu. (*Anasimama.*) Loo! Heshima yangu jamani. Heshima yangu ivunjwe katika miaka ya uzee wangu. Ala-la-la-la !

Mama Salum: (*Kwa hasira*) Kama hutaki kusema lililotokea, toka nyumbani kwangu. Toka nakwambia. Kwanza sijui kwa nini nimekukaribisha. Kwa hiyo kama hutaki kumaliza shida zako nenda, bwana, tafadhali.

Mzee Isa: Aaa! Tusigombane, mama. Ugomvi wa miaka mingi iliyopita usirudishwe leo. Lakini kwa nini kurefusha mambo? Ngoja nikueleze jambo lenyewe niuone huo ukali wako unaojivunia utaishia wapi. Salum amefanya mapenzi na mwanangu, Rukia, na wanapanga kuoana.

Mama Salum: (*Anashika mikono kichwani, anasimama na kutembeatembea chumbani.*) Mama wee!

Mzee Isa: Kuomboleza kutafaa nini, mama. Tukae chini tushauriane la kufanya. Umwambie mwanao, Salum, aache upuuzi huu. Walahi heshima yangu.

Mama Salum: (*Kwa hasira*) Ala-ala-ala! Unasema nini? Mwanangu Salum? Na wewe je? Aa, Mungu huyu! Miaka ishirini na tano (mitano) nimebeba mzigo wa aibu

peke yangu. Ulifaulu kunitisha nisyaseme mambo haya. Sikuwa na la kufanya ila kunyamaza lakini leo Mungu mwenyewe akakueleza. Haya baba, tukuone ujanja wako utaishia wapi. (Uk. 17).

Salum darf nicht wissen, daß er der Sohn Mzee Isas ist. Da es ihnen beiden gelungen ist, das fünfundzwanzig Jahre lang zu verheimlichen, warum soll es jetzt nicht möglich sein, meint Mzee Isa.

Mama Salum: (Anacheka.) Wasema juu ya heshima saa hizi. Heshima unajua wewe. Mimi siijui hata siku moja. Miaka yote hii nimeishi kwenye aibu ya kuwa na mtoto asiye na baba. Heshima yangu ulivunja wewe zamani sana. Sasa sielewi kwa nini unataka mimi nikusaidie kusitiri heshima yako. Yaangalie wewe mwenyewe.

Mzee Isa: Tusifanye mzaha.

Mama Salum: Mzaha unafanya wewe. Kwako heshima ni bora kuliko kuwaacha watoto waoane wakiwa ndugu. Lakini mimi, nikwambie wazi kabisa, sitamwachilia mwanangu aoe dada yake. Ndiyo maana alijawa na wasiwasi mkubwa. Umeshamwambia kuwa Rukia ni dada yake?

Mzee Isa: La, hash! Ila nimemkanya vikali asiendelee kufanya mapenzi na Rukia.

Mama Salum: Sababu gani umempa kuhusu kumkataza.

Mzee Isa: Ala! Heshima yangu. (Uk. 18).

Salum tritt ein.

Mama Salum: (...) Ehe! Afadhali umefika, baba! Hebu nieleze sasa, Mzee Isa amekupa sababu gani kukukataza usifanye mapenzi na Rukia. (*Salum anamtazama Mzee Isa na kunyamaza.*) Sema, mwanangu, nimeshasikia habari zote. Jibu swali langu hilo moja.

Salum: Sina baba, kwa hiyo sitakuwa na mtu wa upande wangu wa kusimamia sherehe za harusi. Jambo hilo eti litamvunja heshima Mzee Isa. Alinikemea sana njiani. Mama, na hata nikiyakumbuka maneno aliyoyasema moyo wangu unataka kupasuka. Lakini sitaki kuyarudia na kama mnagombana hapa juu ya jambo hilo sitaki kuyasikia maneno yaliyokwisha semwa. Mama, ninaloomba (ninaloliomba) ni moja tu. Mzee Isa ananikatalia binti yake ambaye mimi naona siwezi kuishi bila naye. Yote hayo kwa sababu sina baba. Ni kweli simjui baba yangu. Lakini, Mama, kama kweli unanipenda sasa hivi – na Mzee Isa akiwepo – niambie baba yangu ni nani. Hata kama alikufa nitakwenda nimwonyeshe Mzee Isa kaburi halafu nitafute baba zangu wadogo au wakubwa ili mradi nipate mtu wa kusimamia sherehe anazozitaka Mzee Isa, na mimi nipate Rukia, maana maisha yangu ni bure bila Rukia. (Uk. 18-19).

Rukia bittet um Einlaß und tritt ein. Sie möchte Mzee Isa nach Hause mitnehmen, denn sie haben Besuch.

Mzee Isa: Nitakwenda basi. (Uk. 19).

Mama Salum lässt aber Mzee Isa nicht einfach gehen.

Mama Salum: Wapi unakwenda? Rudi Mzee Isa, haya maneno yaishie hapa. Siwezi tena kubeba uchungu huu moyoni mwangu. Nitakufa siku zangu bado. (*Salum*

na Rukia wanashangaa.) Zamani ulinitisha kuniua basi nikanyamaza nikiogopa kuwa nikifa nani atanitunzia mwanangu, Salum. Lakini leo nitaogopa nini? Hata ukiniua mimi ni mzee sihitaji cha zaidi kwenye maisha na mwanangu niliyeishi kwa ajili yake ni mtu mzima anaweza kujiangalia¹¹. Kama ni heshima unayolilia wewe mimi siifahamu. Kwa hiyo siogopi kusema. Kama kudanganya watu na kutesa wengine ndiyo heshima unayoidhamiri wewe basi mimi leo niko tayari kuivunjilia mbali. Hukuijua maana ya heshima toka mwanzo wala hujui sasa na sioni kwa nini ujidanganye wewe pamoja na watu wengine kuwa una heshima ya kujivunia. Salum mwanangu ningekuwa sikupendi mimi usingeishi kufikia umri ulio nao lakini ni upendo huo huo utakaokuletea huzuni ya muda lakini ya haki kwa sababu itakuponya kutoka balaa na kukupa heshima ya haki. Huwezi kumwoa Rukia. Baba yako huyu hapa – Mzee Isa. (*Uk. 19*).

Alle schauen einander an. Niemand traut sich ein Wort zu sprechen.

Tamati

¹¹ Anglizismus „*look after yourself*“. Diese Generation von Swahili-Autoren hatte ihre Schulausbildung auf Englisch gehabt. Besser wäre „*kujitunza*“ oder „*kujitegemea*“.